# RUANGWA DC

RUANGWA KWA MAENDELEO INAWEZEKANA TIMIZA WAJIBU WAKO

Kitengo cha Habari na Mawasilino Serikalini

JARIDA Toleo namba 02 Julai 2024 Tetembelea www.ruangwadc.go.tz ruangwadc

HALIUZWI




Pg 13 >>>

## Mhe. Majaliwa Achangisha Milioni 928.67 Ujenzi wa Kanisa Kuu katoriki Jimbo la Lindi



Pg 12 >>>

## DC Ngoma Afanya Kikao na Wafanyabiashara Ruangwa





Pg 12 >>>

## Chikongwe: Fanyeni Kazi kwa Bidii



Pg 19 >>>

## Mkuu wa Mkoa wa Lindi Awaombea Dua wafanyabiashara Ruangwa



Pg 04 >>>

## Mkurugenzi Chonya Afungua Mafunzo ya Mtaala Mpya kwa Shule za Sekondari Ruangwa

# Yaliyomo

| | |
|---|---|
| *Maelfu Wajitokeza Kwenye Ufunguzi Wa Mafunzo ya Usambazaji Matokeo ya Sensa Ruangwa* | 3 |
| *Mkurugenzi Chonya Akabidhiwa Vifaa Vya Tehama kwa Ajili ya Shule za Sekondari Ruangwa* | 4 |
| *Vijiji vya Nanjaru na Nambiranje Vyapewa Elimu ya Kujiki nga na Magon jwa ya Mlipuko* | 5 |
| *Wilaya ya Ruangwa Yaazimisha Siku ya Mashujaa kwa Kufanya Usafi Soko Kuu* | 6 |
| *Mkurungenzi Chonya Atimiza Nadhiri Yake kwa Mchungaji wa E.A.G.T Ruangwa* | 6 |
| *Kata ya Nachingwea Yaongoza Kuwa na Idadi Kubwa ya Watu Ruangwa* | 7 |
| *Mkurugenzi Chonya Afanya Kikao cha Kamati ya Uhakiki Madeni ya Halmashauri* | 8 |
| *Kamati ya 'KASEMA' Yazinduliwa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa* | 9 |
| *Kambi Maalum ya Matibabu ya Macho Ruangwa Yafanikiwa Kwa Kishindo* | 9 |
| *Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Afanya Kikao na Wananchi wa Kijiji cha Mbangala* | 10 |
| *Waziri Mkuu: Rais Samia Amedhamiria Kufiki sha Huduma za Kijamii Maeneo Yote Nchini* | 11 |
| *Mkurugenzi Chonya Afungua Mafunzo ya Mtaala Mpya kwa Shule za Sekondari Ruangwa* | 11 |
| *Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Afanya Kikao cha Kusikiliza Kero za Wafanya biashara* | 12 |

# Yaliyomo

*Hakuna Mafanikio ya Miujiza Lazima Ufanye Kazi- Chikongwe* 12

*Harambee ya Ujenzi wa Kanisa Kuu Tarajiwa la Mt. Andrea Kagwa la Jimbo Katoliki la Lindi* 13

*Wazazi Ruangwa Waombwa Kuwaruhusu Watoto Kuonesha na Kukuza Vipaji Vyao* 14

*Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii 872 Kupatikana Ruangwa* 15

*Taasisi za Kifedha Wilaya ya Ruangwa Zaombwa Kuwakwamua Wakulima Kiuchumi* 16

*Mwenyekiti wa Halmashauri Afanya Ziara ya Kuwatembelea Wafugaji wa Kuku Kata ya Nandagala* 17

*Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam Tawi la Ruangwa Kukamilika Ndani ya Miezi 18* 18

*Mkuu Wa Mkoa wa Lindi Awaombea Dua wafanyabiashara Ruangwa* 19

*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Akagua Kituo cha Askari wa Uhifadhi Wanyamapori Ruangwa* 19

*Dondoo za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi* 20

*Matukio Katika Picha* 21

*Kongamano la Kukusanya Maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 Wilaya ya Ruangwa Lafanyika Leo* 22

*Vijiji Vyote 90 vya Wilaya ya Ruangwa Vina Umeme Sasa* 23

*Wazazi Wilaya ya Ruangwa Wasisitizwa Kuwapa Watoto Wao Elimu* 23

*Tanzia* 24





# Maelfu Wajitokeza Kwenye Ufunguzi Wa Mafunzo ya Usambazaji Matokeo ya Sensa Ruangwa

Wananchi kutoka Wilaya ya Ruangwa, Nachingwea na Liwale wamejitokeza kwa wingi kushiriki Ufunguzi wa Mafunzo ya Usambazaji na Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya mwaka 2022 kwa Viongozi, Watendaji na makundi mbalimbali.

Ufunguzi huo umefanyika leo Julai 2, 2024 katika viwanja vya Kilimahewa wilayani Ruangwa, mkoani Lindi ambapo mgeni rasmi amekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Aidha, Mhe. Kassim Majaliwa. Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amesema matokeo ya sensa yanapaswa yawafikie watendaji na walengwa wote katika ngazi ya mkoa na Halmashauri na yawe msingi wa rejea katika kufanya maamuzi yote ya kibajeti, kupanga miradi ya maendeleo na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kisekta.

Ametoa agizo hilo leo (Jumanne, Julai 2, 2024) wakati akizungumza na viongozi, wananchi na wadau mbalimbali waliohudhuria ufunguzi wa Mafunzo ya Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa Viongozi na Watendaji wa Halmashari za Wilaya za Liwale, Nachingwea na Ruangwa mkoani Lindi uliofanyika kwenye viwanja vya Maonesho, Kilimahewa mjini Ruangwa.

Amesema usambazaji na mafunzo ya matumizi ya matokeo ya sensa viwe ni ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya kikanuni katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri. “Watendaji wote myabebe haya matokeo mkayatumie, muwe viongozi wa kuhakikisha yanatumika.”

Amewataka viongozi na watendaji wakae pamoja na kutafakari namna bora ambayo matokeo ya sensa yanaweza kutumika kubadili hali za maisha ya wananchi pamoja na kuhimiza uwekezaji. “Matokeo haya yanapaswa yatumike na yasaidie kubadilisha maisha ya wananchi huku mkijua kwamba fedha nyingi zimetumika kuifanya kazi hiyo,” amesema.

Akitolea mfano Mkoa wa Lindi, Waziri Mkuu ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa amesema: “Mkoa wa Lindi una fursa nyingi za kuvutia uwekezaji hivyo ni wakati sasa wa kutumia matokeo haya ya sensa kuitangaza Lindi na kuibadili kupitia uwekezaji.”

Amewataka viongozi hao waifanye kazi ya kuhuisha anwani za makazi na kuweka mikakati ya kutunza miundombinu yake kuwa ni endelevu kwa ajili ya kurahisisha ufikiwaji wa wananchi, kurahisisha biashara mtandao, uwekezaji na uwajibikaji. “Kila Halmashauri nchini, ifanye uhakiki wa vibao vilivyowekwa, waelimisheni wananchi umuhimu wa matokeo hayo ili yawasaidie.

# Mkurugenzi Chonya Akabidhiwa Vifaa Vya Tehama kwa Ajili ya Shule za Sekondari Ruangwa






*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonwa pili (Kushoto) akikabidhiwa vifaa vya TEHAMA na Kampuni ya Reneal International Education Outreach leo Julai 6, 2024 katika ofisi za Halmashauri.* **Picha na mpiga picha wetu.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonya amekabidhiwa vifaa vya TEHAMA na Kampuni ya Reneal International Education Outreach chini ya Mkurugenzi Ndugu David Nyangaka zitakazotumika katika shule za Sekondari wilayani Ruangwa.

Vifaa hivyo vimekabidhiwa leo Julai 6, 2024 na Juma Mshihiri ambaye ni fundi wa vifaa vya TEHAMA kwa niaba ya Mkurugenzi wa Kampuni hiyo.

Aidha, vifaa hivyo ni pamoja na Komputa mpakato (Laptop) 100, Vihifadhia nukuu na vifaa vya kujifunzia (Server) 5, vifaa vya kutunza umeme (UPS) 5, na vifaa vya kudhibiti umeme (Regulator) 5.

Shule zilizokabidhiwa vifaa vya TEHAMA ni tano zenye kidato cha tano na sita kwa Wilaya ya Ruangwa, ambazo ni shule ya Sekondari Hawa Mchopa, Lucas Malia, Nkowe, Ruangwa na Mbekenyera.

Katika hatua nyingine, Ndugu Frank Fabian Chonya amewataka Wakuu wa shule hizo kujenga vizuri vyumba maalumu kwa ajili ya matumizi ya komputa mpakato hizo ili wanafunzi waweze kuvutiwa kuingia kujisomea.

Aidha, Ndugu Chonya amesisitiza kwa kusema kuwa komputa mpakato hizo zitumike vizuri na zitunzwe ipasavyo ili ziweze kupandisha ufaulu wa wanafunzi katika Wilaya ya Ruangwa.

"Kwa msaada wa hizi Laptop, Ruangwa sasa tunaenda kuwa namba moja kitaifa kwa ufaulu wa Kidato cha sita" amesema Chonya.

Naye, Mkuu wa shule ya Sekondari Lucas Malia Gladness Makongwa kwa niaba ya Wakuu wa shule za Sekondari zilizonufaika na vifaa hivyo vya TEHAMA ameishukuru Kampuni ya Reneal International Education Outreach kwa msaada huo na kumuahidi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kuyatekeleza yale yote aliyoyaagiza kwao ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Katika Wilaya ya Ruangwa

# Vijiji vya Nanjaru na Nambiranje Vyapewa Elimu ya Kujikinga na Magonjwa ya Mlipuko

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Ndugu Frank Chonya, pamoja na Mganga Mkuu wa Wilaya, Dkt. Feisal Said, wakiambatana na wataalamu wengine wa Wilaya, wamefanya ziara maalum ya kutoa elimu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko katika vijiji vya Nambiranje na Nanjaru, vilivyopo kata ya Nambiranje leo Julai 7,2024.

Ziara hiyo ililenga kuwapa wananchi elimu juu ya njia bora za kujikinga na magonjwa ya mlipuko. Mkurugenzi na timu nzima ya wataalamu walitembelea vyanzo vyote vya maji vinavyotumiwa na wananchi, ambapo wataalamu wa afya waliweka dawa za kuua vijidudu (Chlorine) ili kuhakikisha maji yanakuwa safi na salama kwa matumizi. Mbali na kuweka dawa kwenye vyanzo vya maji, Maafisa Afya wa Wilaya wamegawa dawa za kutibu na kusafisha maji (waterguard) kwa wananchi







ili kuhakikisha maji wanayotumia nyumbani kwaajili ya kunywa yanakuwa safi na salama muda wote.

Aidha, Ndugu Chonya amewasisitiza wananchi kuzingatia usafi wa maji, vyakula wanavyokula, na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni. Amewataka wananchi kuhakikisha wanajisaidia chooni ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kama vile kuhara na kutapika, ambayo husababishwa na kujisaidia ovyo kwenye mazingira.

Sambamba na hayo, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dkt. Feisal Said, ameongeza kwa kusisitiza umuhimu wa kujisaidia chooni na akatoa maelezo ya jinsi magonjwa ya kuhara yanavyosababishwa na kula au kunywa chakula kilichochanganyika na kinyesi kupitia nzi au maji machafu.

"Hakikisheni mnajisaidia chooni maana hakuna namna nyingine ya mtu kupata magonjwa ya kuhara isipokuwa kwa kula kinyesi. Nzi anaweza kubeba kinyesi na kuweka kwenye chakula au mvua kutitirisha kinyesi mpaka kwenye maji mnayotumia kwa kunywa, na hapo ndipo utajikuta unapata madhara," amesema Dkt. Feisal. Kwa upande wao, uongozi wa RUWASA umeleza kuwa Serikali imetenga bajeti ya mradi wa maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mradi huo utaanza kutekelezwa mara moja baada

ya mchakato mzima wa utekelezaji mradi huu kukamilika, ili kuhakikisha wananchi wa kata ya Nambiranje wanapata maji safi na salama.

**"Matokeo ya Sensa yanapaswa yawafikie Watendaji na walengwa wote katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri na yawe msingi wa rejea katika kufanya maamuzi yote ya kibajeti, kupanga miradi ya maendeleo na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kisekta.**

**MHE. MAJALIWA WAZIRI MKUU**

# Wilaya ya Ruangwa Yaazimisha Siku ya Mashujaa kwa Kufanya Usafi Soko Kuu





*Viongozi na wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wakijumuika kwa pamoja kufanya usafi kwenye eneo la soko kuu la Wilaya ya Ruangwa leo Julai 25, 2024, ikiwa ni moja ya hatua za kuadhimisha siku ya Mashujaa Tanzania. siku ya mashujaa inaadhimishwa nchini Tanzania julai 15 kila mwaka ili kuwaenzi mashujaa waliopigania uhuru.Picha na Mpigaga picha wetu*

Viongozi na wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wajumuika kwa pamoja kuadhimisha siku ya Mashujaa Tanzania kwa kufanya usafi Soko kuu Ruangwa leo Julai 25, 2024 saa 12 asubuhi.

Siku ya Mashujaa nchini Tanzania, ambayo huadhimishwa tarehe 25 Julai kila mwaka, ina historia yake iliyojaa heshima na kumbukumbu kwa mashujaa wa taifa hili. Hii ni siku ya kuwakumbuka na kuwaenzi wale wote walioopigania Uhuru na haki za wananchi wa Tanzania, pamoja na wale waliotoa maisha yao kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Siku hii ilianzishwa rasmi baada ya Tanzania kupata Uhuru wake kutoka kwa nchi ya Uingereza mwaka 1961, na ni siku muhimu katika kalenda ya Taifa kwa ajili ya kuwapa heshima mashujaa wa vita mbalimbali na harakati za ukombozi.

Pia ni siku ya kutafakari kuhusu mchango wa wanajeshi, polisi, na wananchi wa kawaida ambao wamefanya kazi kubwa katika kulinda na kuendeleza amani na Uhuru wa Tanzania.

Katika maadhimisho haya, Serikali pamoja na wananchi hufanya shughuli mbalimbali kama vile kumbukumbu maalum, maombi, na sherehe za kitaifa zinazoambatana na hotuba za viongozi wakuu wa nchi.

Nazo, familia za mashujaa hupokea heshima maalum na zawadi kama ishara ya kutambua mchango wao mkubwa kwa Taifa. Kwa mwaka huu maadhimisho haya kitaifa yanafanyika mkoani Dodoma

## Mkurugenzi Chonya Atimiza Nadhiri Yake kwa Mchungaji wa E.A.G.T Ruangwa



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonya atimiza nadhili yake kwa Mchungaji wa kanisa la EAGT Ruangwa

Michael Kisasa kwa kumpatia pikipiki aina ya Sino Ray ikiwa "full tank" ambayo itarahisisha utendaji kazi wake wa kueneza neno la Mungu kwa waumini.

Nadhili hiyo ameitimiza leo Julai 21, 2024 katika ibada ya Jumapili na kutoa kwa waumini wa Kanisa hilo ya kwamba kwa Mungu hakuna masikini hivyo mtu ukiwa nacho hata kidogo basi saidia kwa wenzako kwani ni moyo na si utajiri. Aidha, Ndugu Chonya amewasisitiza waumini hao kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kikamilifu zoezi ambalo linaanza na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ambalo limezinduliwa jana Julai 20, mkoani Kigoma na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa.

Kwa upande wake, Mchungaji Kisasa amemshukuru Mkurugenzi na familia yake kwa kujitoa kwao katika mambo mbalimbali yanayohusisha jamii.

# Kata ya Nachingwea Yaongoza Kuwa na Idadi Kubwa ya Watu Ruangwa




Kwa mujibu wa Takwimu za Matokeo ya Sensa ya watu na makazi 2022 Kata ya Nachingwea wilayani Ruangwa inaongoza kuwa na idadi ya watu wengi ikiwa na watu 18,343 ikifuatiwa na Kata ya Mbekenyera yenye watu 16,531, Kata ya Nandagala ikiwa na watu 7391, huku Kata ya mwisho ikiwa ni Makanjiro yenye watu 4002 na kufanya Wilaya ya Ruangwa kuwa na julma ya watu 185,573.

Aidha, Matokeo ya Sensa ya watu na makazi imeonesha uwiano wa watu kwa jinsia idadi ya Wanaume kwa kila Wanawake 100 ambapo kwa Wilaya ya Ruangwa ina uwiano ya Wanaume 97 kwa kila Wanawake 100.

Na katika Kata za Wilaya ya Ruangwa Kata inayoongoza kwa kuwa uwiano wa juu wa jinsia kati ya Wanaume na Wanawake ni Kata ya Mbwemkuru, Machang'anja,Nambilanje, Mbekenyera, Matambarare na Chibula na hii inaonesha kwamba Wanaume ni wengi kuliko Wanawake.

Kata ya Namichiga na Chienjele uwiano wa jinsia kati ya Wanaume na Wanawake ni 100 kwa 100 na Kata ya Nandagala uwiano wa jinsia ni Wanaume 93 kwa Wanawake 100, na Kata ya Mnacho ina uwiano mdogo wa watu kwa jinsia kwa kuwa na Wanaume 91 kwa Wanawake 100.

Katika upande wa Idadi ya Kaya katika Wilaya ya Ruangwa ina jumla ya Kaya 60931 na Kata ambayo inaongoza kwa idadi kubwa ya Kaya ni Kata ya Nambilanje ambayo inaongoza kwa wastani mkubwa wa watu kwa Kaya ina wastani wa watu 3.5, Mbwemkuru wastani wa watu 3.3, Nandagala wastani wa watu 3.0 na Mnacho wastani wa watu 2.8.

Sensa ya watu na makazi 2022 aidha imeonesha idadi ya watoto chini ya umri wa miaka 18 ambapo kwa Wilaya ya Ruangwa ina 37% ya watoto chini ya miaka 18. Na Kata inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto chini ya miaka 18 ni Kata ya Nambilanje 40.3%, Mbwemkuru 40.0%, Nandagala ina 35.6%, na Mbekenyera ina 34.4%.

Takwimu za idadi ya Vijana kuanzia umri wa miaka 15-35 katika Wilaya ya Ruangwa ni 34.6% ambapo Kata ya Nachingwea inaongoza kuwa na vijana wengi zaidi ya 40.9%, Mbekenyera ni 38.5%, Nandagala ni 33.6% na Malolo ina asilimia ndogo ya Vijana ambayo ni 30.4 ukilinganisha na Kata zote wilayani humo.

> **Katika kuhakikisha huduma za Afya zinakuwa karibu zaidi na wananchi Serikali imejipanga ambapo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa tunatarajia kupata Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii 872**
>
> Bi.Orsolina Tolage

**SIKILIZA RUANGWA FM 88.4**

RUANGWA FM



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Chonya (Kulia) akiwa kwenye Kikao maalum cha kamati ya kuhakiki madeni ya Halmashauri leo Julai 8, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkurugenzi. lengo la kutoa elimu ya madeni kwa jamii . picha na mpiga picha wetu*

# Mkurugenzi Chonya Afanya Kikao na Kamati ya Kuhakiki Madeni ya Halmashauri

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonya amefanya Kikao na Kamati ya kuhakiki madeni ya Halmashauri leo Julai 8, 2024 katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mkurugenzi.

Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti Hosea Shibanda ilianzishwa kwa lengo la kutoa elimu ya madeni kwa jamii, kupata idadi kamili ya wadai ili kuwaweka katika bajeti ya mwaka huu wa fedha na kuweka utaratibu maalum wa kuwalipa wadai hao, pia kuhakiki na kufahamu madeni yenye uhalisia ya wadai ili mwaka huu wa fedha wadai wawekwe kwenye bajeti.

Kamati ilianza ziara yake Machi 11, 2024 katika Kata zote 22 zilizopo wilayani Ruangwa na kuhakiki madeni kwa watumishi wa Serikali, Wazabuni, Wakandarasi, na wananchi wote na kupata jumla kuu ya madeni ya wadai ni shilingi 1,759,909,726.

Katika hatua nyingine, Ndugu Chonya ametoa maagizo kwa Kamati ya kuhakiki madeni ili kuiboresha zaidi, Kamati ipitie vizuri madeni ya Watumishi na kukaa na Afisa utumishi, Kamati ikutane na Mhandisi ili kupitia madeni ya Wazabuni hadi kwa wale ambao bado hawajajiorodhesha, Kamati iorodheshe watu wanaodaiwa na Halmashauri kama vile watu wa kodi mbalimbali, Kamati ikae na muweka hazina,

Mkaguzi wa ndani na Mhasibu ili kujua ni madeni gani ambayo tayari yameshalipwa, pia Kamati ikae na Wakuu wa idara zote ili kujua Watumishi wanaoidai Halmashauri.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wilaya ya Ruangwa Ndugu Thabit Wailala ameishukuru Kamati kwa ushirikiano mkubwa na kufanya kazi kwa ufanisi na weredi mkubwa.

# Kamati ya 'KASEMA' Yazinduliwa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe amezindua Kamati ya "Kasema" itakayoshirikiana na Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumi unaoongozwa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM).

Uzinduzi huo umefanyika leo Julai 9, 2024 katika Kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri.

Kamati ina Wajumbe watano na ina lengo la kukusanya na kushughulikia maoni au malalamiko ya wananchi katika eneo husika kuhusu Mradi.

Pia, ina lengo la kuweka kumbukumbu za kile kinachofanyika katika Mradi, na ni sehemu ya Ulinzi na Usalama wa Mradi huo.

Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumu chini ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam umefadhiliwa na Mkopo wa Benki ya Dunia na utekelezaji wake ni katika maeneo mapya 14, na mpaka sasa maeneo mapya matatu tayari yameshafikiwa ambayo ni Ngongo(Lindi Manispaa), Likunja( Wilaya ya Ruangwa) pamoja na Kagera.

Katika hatua nyingine, Mhe. Chikongwe ameupongeza Uongozi wa Kata ya Likunja kwa kutoa Hekari 400 ambapo Kitivo cha Kilimo kitajengwa.Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo ambaye ni Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumu Profesa Bernadeta Killiani ametoa wito kwa wananchi wa Ruangwa kutoa ushirikiano kwani mafanikio ya Mradi itategemea muamko na ushirikiano wa wananchi wenyewe







*Picha mbalimbali za Uzinduzi wa kamati ya KUSEMA inayokusanya maoni ya utekelezaji wa mradi wa HEET unaotekelezwa Wilaya ya Ruangwa uzinduzi huo umefanyika leo Julai 9, 2024 katika Kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri.*




*Dakitari bingwa wa Magonjwa ya macho Dkt. Mwita Machage akiendelea na zoezi la upasuaji wa macho katika Kambi maalum kwa ajili ya matibabu ya macho iliofanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa kuanzia tarehe 8 Julai 2024 hadi Julai 19, 2024, Kambi hiyo ilikuwa na lengo la kusogeza huduma ya upasuaji wa macho kwa wananchi.* **picha na mpiga picha wetu**

# Kambi Maalum ya Matibabu ya Macho Ruangwa Yafanikiwa Kwa Kishindo

Kambi maalum kwa ajili ya matibabu ya macho imefanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa kuanzia tarehe 8 Julai 2024 hadi leo Julai 19, 2024, Kambi hiyo yenye lengo la kusogeza huduma ya upasuaji wa macho kwa wananchi, imeandaliwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na shirika la Eye Corps, lenye makao yake makuu nchini Marekani.

Katika kambi hiyo, wagonjwa 728 wamepata huduma za uchunguzi wa macho, kati yao wagonjwa 272 wamefanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho. Upasuaji huo umefanywa na Madaktari bingwa kutoka Tanzania, India, na Marekani. Huduma hii imetolewa bila malipo yoyote kwa wagonjwa, hatua ambayo imepokelewa kwa shukrani kubwa na jamii, ikumbukwe shirika la Eye Corps limeingia ubia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa huduma za matibabu ya macho katika Mikoa mbalimbali ikiwemo Lindi, Kilimanjaro na Songea

Aidha, Dkt. Mwita Machage, ambaye ni Mratibu wa Huduma za Macho Mkoa wa Lindi kutoka Hospitali ya Rufaa ya Sokoine, ameeleza jinsi huduma hiyo ilivyofanikiwa

kuwafikia watu wengi, lakini pia amehimiza watu kujenga tabia ya kupima macho mara kwa mara, ili kufahamu afya ya macho yao. Pia, ametoa shukrani kwa wananchi wa Ruangwa kwa kujitokeza kwa wingi kupima macho na kupata matibabu.

Sambamba na hayo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Dkt. Feisal Said, ameishukuru Serikali kwa kuwezesha huduma hiyo iliyodumu kwa siku 11 na kufanikisha kurudisha furaha kwa wakazi wengi wa Ruangwa.

“Kambi hii imesaidia sana maana wagonjwa walikuwa wanasafiri kwenda hospitali ya Mkoa lakini kwa sasa imewapunguzia gharama kwa kupata huduma hapa hapa hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, huduma hii imesaidia sana na imefanikiwa kuwafikia watu wengi katika Wilaya yetu,” amesema Dkt. Feisal.

Kwa upande wao, baadhi ya Wananchi waliopata huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho, Bi. Zainabu Thomas na Bi. Yasmin Seleman wameishukuru sana Serikali kwa huduma

waliyopata. Wamesema walikuwa hawawezi kuona kabisa lakini kwa sasa wanaona. Walikuja hawawezi kutembea bila kushikwa mkono baada ya upasuaji wameweza kutembea wenyewe, hivyo basi wanashukuru sana kwa msaada huo wa matibabu, ambao umewasaidia kupona matatizo ya macho.

# Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Afanya Kikao na Wananchi wa Kijiji cha Mbangala



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Tanzania Mhe. Dunstan Kitandula akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mbangala*



*Wananchi wa kijiji cha Mbangala wakiwa kwenye kikao na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii leo Julai 17, 2024.*

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Tanzania Mhe. Dunstan Kitandula, amefanya kikao na wananchi wa kijiji cha Mbangala kilichopo Kata ya Makanjiro wilayani Ruangwa.

Kikao hicho kimefanyika leo Julai 17, 2024 kikiwa na lengo la kusikiliza kero, changamoto, na kutoa elimu juu ya athari zinazosababishwa na wanyama pori, hususani Tembo, katika kijiji hicho.



*Wananchi wa kijiji cha Mbangala wakiwa kwenye kikao na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii leo Julai 17, 2024.*

washukuru wananchi wa Mbangala kwa uwazi wao katika kueleza matatizo wanayokabiliana nayo na amewahakikishia kwamba Serikali ipo bega kwa bega na wananchi katika kutatua changamoto hiyo. Amesisitiza uvumilivu kutoka kwa wananchi kwani Serikali iko kazini kutafuta suluhisho la kudumu.

Katika hatua nyingine Mhe. Kitandula ameleza kwamba Serikali imejipanga kununua helikopta mbili zitakazotumika katika zoezi la kuondoa Tembo karibu na makazi ya watu.

Sambamba na hayo, Mhe. Kitandula amesema kuwa Serikali imepokea maombi 377 ya kifuta machozi kutoka kwa wananchi waliokumbwa na matatizo ya Tembo kutoka Wilaya ya Ruangwa na imeahidi kuyashughulikia haraka na kuhakikisha wale wanaostahili wanalipwa fidia zao.

“Ninapata machungu kama mnayopata ninyi maana naelewa nini mnapitia kwa wakati huu, Serikali itashughulikia kero zote na ni suala la muda tu, pia mnatakiwa kufahamu kwamba shughuli za binadamu zimefika mpaka kwenye maeneo ya hifadhi za wanyama na kuwafanya wanyama kutoka kwenye makazi yao. Mfano, zamani Tanzania ilikuwa na Tembo 300,000 lakini hakukuwa na vurugu kama hizi za sasa ambapo tuna tembo 60,000 na tatizo limekuwa kubwa sana” amesema Mhe. Kitandula.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma, ameishukuru Serikali kwa msaada na jitihada za kudhibiti tatizo la Tembo katika kijiji cha Mbangala.

“Serikali inafanya kazi nzuri sana kila tukihitaji msaada wataalamu wanafika mapema sana na kutusaidia, kipekee nikushukuru Mhe. Naibu Waziri kwa ujio wako najua utatusaidia kupata majawabu ya wanambangala” amesema Mhe. Ngoma.

Nao, wananchi wa Kijiji cha Mbangala wametoa maoni, kero na mapendekezo yao kwa Serikali, wakieleza kuwa Tembo wanaleta umasikini kwa kuharibu mashamba yao na kuiomba Serikali kuchukua hatua zaidi kudhibiti tatizo hilo.



*Bw. Juma Ngutai Mkazi wa kijiji cha Mbangala akitoa maoni kwenye kikao cha Naibu Waziri wa Maliasili leo 17-07, 2024.*

# Waziri Mkuu: Rais Samia Amedhamiria Kufiki sha Huduma za Kijamii Maeneo Yote Nchini



*Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na Wakazi wa Kijiji cha Mmawa Kilichopo kata ya Nandagala Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi leo Julai 3, 2024. alipo kuwa kwenye ziara maalum kijijini hapo.*

**Mhe. Kassim Majaliwa**

**WAZIRI MKUU WA TANZANIA**
**MBUNGE JIMBO LA RUANGWA**

Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa Mhe. Kassim Majaliwa leo Julai 3, 2024 amezungumza na wakazi wa kijiji cha Mmawa kilichopo katika kata ya Nandagala, Ruangwa Mkoani Lindi. Akizungumza na Wakazi hao Mheshimiwa Majaliwa amesema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuendelea kufikisha huduma za jamii ikiwemo Afya, maji, Umeme na Elimu katika maeneo yote nchini.

"Kwa mfano katika Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea tuna mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 119, kwa mradi huu maeneo mengi hapa yatapata huduma ya maji. Rais Dkt. Samia pia aliamua kununua mitambo ya kuchimbia visima vya maji lengo ni kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwenye maeneo yetu."

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa amewataka maafisa kilimo nchini kuweka mpango wa kuwahamasisha na kuwasimamia vijana kuingia katika kilimo cha bustani kwenye maeneo ya mabonde yanayofaa kwa kilimo.

# Mkurugenzi Chonya Afungua Mafunzo ya Mtaala Mpya kwa Shule za Sekondari Ruangwa



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa amefungua mafunzo ya Mtaala mpya kwa shule za Sekondari Elimu ya Juu (Curricullum for Upper Secondary Education) leo Julai 8, 2024 katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Ruangwa.

Mafunzo haya yatafanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia leo Jumatatu mpaka Jumatano na kuhusisha Walimu wa shule tano zenye wanafunzi wa kidato cha tano na sita na ni kufuatia maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati alihutubia Bunge baada ya kuapishwa kwake kuwa Rais mwaka 2021 na kuiagiza Wizara ya Elimu kupitia upya Mitaala kama inakidhi vigezo na uhitaji wa wanafunzi.

Aidha, Ndugu Chonya amewataka Walimu kusikiliza kwa makini, kuwa watulivu ili wajifunze kikamilifu na wasisite kuuliza pale wasipoelewa, ili wanavyorudi kuwafundisha wanafunzi shuleni wafundishe kadri Mtaala unavyotaka.

Pia, amemuagiza Afisa Elimu Sekondari Ndugu Ernest Haule kuwapa posho Walimu wanaoshiriki mafunzo hayo ili kujikimu kwa siku hizi 3 za mafunzo.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mafunzo hayo Ndugu Ali Juma kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), ameushukuru uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa mapokezi mazuri na kutoa wito kwa walimu kuyazingatia yale watakayofundishwa ili kukuza sekta ya Elimu Tanzania.

## Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Afanya Kikao cha Kusikiliza Kero za Wafanyabiashara



Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma amefanya Kikao cha kusikiliza kero za Wafanyabiashara wa Ruangwa leo Julai 12, 2024 katika Ukumbi wa Chama cha Walimu wilayani Ruangwa na kuwaahidi ya kwamba kero zao zinakwenda kutatuliwa.

" Naenda kuyafanyia kazi malalamiko yenu na ninawaahidi kuwa baada ya wiki mbili yatakuwa yamekwishwa, kwani ninajua Wafanyabiashara ndio mnaoendesha uchumi wa Wilaya, Mkoa na nchi kwa ujumla" Amesema Ngoma.

Miongoni mwa kero zilizobainishwa na Wafanyabiashara hao ni pamoja na lugha isiyo rafiki kutoka kwa Maafisa wakusanya kodi, ukadiliwaji wa juu wa kodi, mazingira yasiyo rafiki kwa ufanyaji wa biashara, kutengewa maeneo ya kutosha kwa ajili ya Wafanyabiashara ndogondogo, kuongezewa muda wa kufanya biashara, kuwepo na utaratibu mzuri wa kukata leseni, kutokuwepo kwa huduma ya vyoo yenye uhakika maeneo ya biashara

Aidha, Mhe. Ngoma ameendelea kwa kusema kuwa Taifa linaendeshwa na kodi, ila sio kodi ya machozi, jasho na damu na kitu chochote cha maendeleo kinachofanywa na Serikali basi hutokana na kodi za Wafanyabiashara



## Hakuna Mafanikio ya Miujiza Lazima Ufanye Kazi- Chikongwe

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ametoa wito kwa wananchi wa Kijiji cha Namahema B kilichopo Kata ya Nandagala wilayani Ruangwa kufanya kazi kwa bidii hususani kwenye kilimo ili kutimiza ndoto zao.

"Hakuna namna ya kubadili maisha yetu kama si kujiimarisha na kujituma kiuchumi, wapo watu wengi wamefanya mambo ya maendeleo kupitia kilimo, tusikidharau kilimo, cha msingi ni kulima kisasa kwani kwenye maisha hakuna mafanikio ya miujiza ni lazima ufanye kazi ndipo ufanikiwe" Amesema Chikongwe.

Ameyasema hayo leo Julai 12, 2024 katika Kikao kazi kilichohusisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Viongozi wa Kata ya Nandagala, Viongozi wa Kijiji cha Namahema B, Viongozi wa Benki ya NMB na Wakulima wa bustani za mbogamboga kutoka Kata ya Nandagala na Mnacho kilichofanyika katika kijiji cha Namahema B.

Aidha, Mhe. Chikongwe amewaomba wananchi wa Kijiji cha Namahema B, kuhakikisha mazingira ya maeneo wanayoishi yanakuwa safi ili kujikinga na magonjwa yanayotokana na uchafu, pia amewataka kufikiria na kubuni biashara mbalimbali ili kuwavutia wawekezaji na kufanya kijiji kinachangamka kimaendeleo. Kwa upande wake mkulima wa bustani za mbogamboga kutoka kijiji cha Ng'au kilichopo Kata ya Mnacho Ndugu Nelson Sweetbert ametoa pongezi kwa viongozi wa Kata ya Nandagala na kuahidi kuyafanyia kazi kwa vitendo yale waliyoagizwa.





# Harambee ya Ujenzi wa Kanisa Kuu Tarajiwa la Mt. Andrea Kagwa la Jimbo Katoliki la Lindi



*Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa ameendesha harambee na kuchangisha sh. milioni 928.67 za ujenzi wa kanisa kuu tarajiwa la Mt. Andrea Kagwa la Jimbo Katoliki la Lindi. Kati ya fedha hizo, sh. milioni 464.3 ni fedha taslimu na nyingine kati ya hizo zimeshawekwa benki na sh. milioni 464.37 bado ni ahadi. Awamu ya kwanza ya ujenzi huo, inatarajiwa kugharimu sh. milioni 700.Akizungumza na waumini na wadau mbalimbali waliohudhuria harambee iliyofanyika Ruangwa mjini, leo mchana (Jumamosi, Julai 27, 2024), Waziri Mkuu amewataka waliotoa ahadi wazikamilishe mapema ili kazi ya ujenzi isikwame.*

















# Wazazi Ruangwa Waombwa Kuwaruhusu Watoto Kuonesha na Kukuza Vipaji Vyao

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mbekenyera iliyopo Kata ya Mbekenyera wilayani Ruangwa Answabu Abdallah Maloi (13) ametoa wito kwa wazazi na walezi kutowakataza watoto wao kuonesha na kukuza vipaji vyao kikubwa ni kuzingatia usalama wao.

“ Watoto tuna vipaji vingi lakini kuna wakati wazazi/ walezi wanatukatisha tamaa na kutufanya vipaji vyetu tusivioneshe kabisa, hivyo basi niwaombe wazazi pindi mnapogundua watoto wenu tuna kitu/ kipaji fulani msituzuie kukionesha na kukikuza pia kwasababu kipaji hicho inaweza ikawa njia ya mafanikio yetu, na watoto tukifanikiwa na nyinyi wazazi mnafanikiwa, kikubwa zingatieni usalama wetu na kukiamini kile tunachokifanya” amesema Answabu

Ameyasema hayo leo Julai 8, 2024 kupitia Redio Jamii, Ruangwa Fm katika kipindi cha “Bodaboda” kinachoongozwa na Mtangazaji Adelina Kaspari.

Mwanafunzi Answabu ameshiriki katika mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania 2024 (UMITASHUMTA) kupitia mchezo wa mpira wa miguu kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa na amechaguliwa katika timu ya Taifa ya vijana chini ya umri wa miaka 17.

Aidha, Answabu ameongeza kwa kusema kuwa mtu yeyote unapofanya jambo usilewe sifa unazopewa na watu wengine kwa mara ya kwanza kikubwa ni kuongeza juhudi ili wakusifie zaidi unavyofanya jambo kubwa na zuri kwako wewe mwenyewe na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake, Afisa Michezo Wilaya Ndugu Shaban Mchinama amewashukuru wazazi wa Answabu kwa kumruhusu mtoto wao kushiriki katika michezo na kutoa wito kwa wazazi wengine waige mfano huu kwani michezo ni afya, urafiki na ajira.

---

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonya ameongoza harambee ya kumpongeza Mwanafunzi wa shule ya Msingi Mbekenyera Answabu Abdallah Maloi (13) ambaye ameshiriki mashindano ya UMITASHUMTA ngazi ya Taifa na kuwa mmoja wapo katika timu ya Taifa ya vijana chini ya umri wa miaka 17.

Harambee hiyo imefanyika leo Juni 8, 2024 katika Kikao cha CMT kilichofanyika katika Ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na kupatikana zaidi ya shilingi 270,000/-

Kwa upande wake, Mwanafunzi Answabu Maloi amewashukuru wote walioijitoa kwa ajili yake na kuahidi atafanya vizuri zaidi kwenye masomo na michezo ili kuongeza hamasa kwa wanafunzi wengine kufanya vizuri zaidi katika sekta ya Elimu na Michezo.



# Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii 872 Kupatikana Ruangwa

Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa Kushirikiana na Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imetoa nafasi 872 kwa wananchi watakaowania nafasi ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi ambao watatambuliwa kupitia Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya ngazi ya jamii.

Akizungumza katika Kikao na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ruangwa leo tarehe 9, 2024 katika Ofisi ya Mkurugenzi, Afisa Mpango wa Taifa wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Bi.Orsolina Tolage kutoka Wizara ya Afya, Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma amesema kila kitongoji kutakuwa na Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wawili.

"Katika kuhakikisha huduma za Afya zinakuwa karibu zaidi na wananchi Serikali imejipanga ambapo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa tunatarajia kupata Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii 872, wawiliwawili kila kitongoji jinsi ya kiume mmoja na jinsi ya kike mmoja , hivyo wataomba nafasi na watachaguliwa kupitia mikutano ya kijiji au mtaa"amesema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Frank Chonya ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuweka kipaumbele suala la Afya hasa kwa kuweka Mkakati wa kuwa na Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika kata 22, vijiji 90 na vitongoji 436 katika Halmashauri hiyo.

"Naishukuru Serikali kwa kuimarisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na hili suala la Mpango Jumuishi wa Wahudumu Ngazi ya Jamii limekuja katika muda mwafaka hivyo tutashirikiana kuhakikisha uchaguzi wa CHW's unafanyika kwa ufasaha.

Ikumbukwe kuwa Uchaguzi wa kuwachagua Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Halmashauri ya Ruangwa unatarajia kuanza mwezi huu ikiwa ni katika Utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Uliozinduliwa na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango tarehe 31,Januari,2024 na lengo ni kupata Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wapatao 137,294 katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Maombi yote yawasilishwe kwa Maafisa Watendaji wa Kata ambao watasimamia zoezi la kuchagua Wahudumu wenye sifa miongoni mwa waliotuma maombi kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa.



*Picha mbalimbali za matukio ya zoezi la kuwachagua wahudumu wa Afya ngazi ya jamii katika Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi Zoezi hilo linahitaji wahudumu wapatao 872 kutoka Vitongoji 436 vya Wilaya ya Ruangwa. Ikumbukwe mchakato mzima wa zoezi hilo umeratibiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Maombi yote yatawasilishwa kwa Maafisa Watendaji wa Kata ambao watasimamia zoezi la kuchagua Wahudumu wenye sifa miongoni mwa waliotuma maombi kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa.*

# Taasisi za Kifedha Wilaya ya Ruangwa Zaombwa Kuwakwamua Wakulima Kiuchumi

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ametoa wito kwa Taasisi ya fedha, Benki ya NMB tawi la Ruangwa kumwezesha mkulima katika nyenzo kwani mkulima akikwamuliwa basi inasaidia hata Benki hiyo kujikwamua kiuchumi.

"Watu wapo tayari kwa kilimo, lakini wanakosa nyenzo, hivyo basi nikuombe Meneja wa Benki ya NMB kuwasaidia wakulima hawa kupata nyenzo zitakazowasaidia kuongeza kasi ya uzalishaji na wewe ni mwenzetu na tuna imani kubwa sana na wewe ya kwamba utatukwamua katika hili" Amesema Chikongwe. Ameyasema hayo leo Julai 12, 2024 katika Kikao kilichofanyika katika Kijiji cha Namahema B kilichopo Kata ya Nandagala wilayani Ruangwa.

Kikao hicho kilihusisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Viongozi wa Kata ya Nandagala, Viongozi wa kijiji cha Namahema B, Viongozi wa Benki ya NMB, na wakulima wa bustani za mbogamboga wa Kata ya Nandagala na Mnacho.

Pia, Kikao kilihusisha kutembelea wakulima wa bustani za mbogamboga akiwemo Ndugu Mohamed Said Chipenya ambaye anajihusisha na kilimo hicho kwa umwagiliaji wa mkono (mashilingwete), Imamu Abeid pamoja na Mussa Nassoro ambao hutumia njia za kisasa katika kilimo hicho cha mbogamboga na kuona utofauti mkubwa uliopo kati ya mkulima ambaye hutumia njia zisizo za kisasa na yule ambaye hutumia njia za kisasa katika kilimo hicho.

Kwa upande wake Meneja wa Benki ya NMB tawi la Ruangwa Ndugu Habibu Moris amesema nia wanayo ya kuwasaidia wakulima kwa sababu kupitia ziara ya kuwatembelea wakulima wamejifunza mengi lakini uaminifu ni silaha kubwa sana katika kufanikisha hayo yote. " Ni kweli mkulima akikwamuliwa na sisi tunakuwa tumejikwamua kwasababu Benki kazi yake ni kuhifadhi akiba za watu, na kutoa mikopo kwa watu, hivyo tunavyoamua kuwakopesha na nyie muoneshe uaminifu kwa kurejesha mikopo kwa wakati ili kuendelea kufanya kazi kwa weredi kama Taasisi, usivyorudisha kwa wakati wengine wanakosa huduma" Amesema Moris

Kijiji cha Namahema B kina jumla ya wakulima 215 ambapo wakulima wa mbogamboga ni 86, wakulima wa Korosho ni 40 na wakulima wa mazao ya chakula ni 89.















# Mwenyekiti wa Halmashauri Afanya Ziara ya Kuwatembelea Wafugaji wa Kuku Kata ya Nandagala

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe amefanya ziara ya kuwatembelea wafugaji wa kuku kutoka kijiji cha Nandagala wilayani Ruangwa ambao ni wanufaika wa mradi wa TPGS akiambatana na Daktari wa Mifugo Kata ya Nandagala pamoja na Mtendaji Kata ya Nandagala.

Ziara hiyo ameifanya leo Julai 14, 2024 ikiwa na lengo la kutoa elimu kwa wanufaika wa mradi huo namna gani bora ya kufuga na faida zake na kutoa wito kwa wafugaji hao kuzingatia namna bora ya ufugaji kwani soko la kuku wa nyama na mayai halijawahi kujaa.

"Mimi niwaambie tu yakwamba hili jambo si dogo na lina manufaa makubwa sana kwenu, soko la kuku wa nyama na mayai halijawahi kujaa, wahitaji ni wengi sana endapo mtazingatia vizuri ufugaji huu, msidharau kabisa au kuishi kwa kutegemea kilimo tu hata ufugaji pia una manufaa kwetu" Amesema Chikongwe.

Mradi wa Tropical Poutry Genetics Solution (TPGS) una lengo la kuendeleza kizazi cha kuku na kuifundisha jamii namna gani nzuri ya kufuga kuku kwa maendeleo endelevu katika familia.

Ili kuendeleza kizazi cha kuku TPGS ina Kituo kikubwa cha chanjo za Mifugo ambapo kipo Arusha na kwa Kanda ya Kusini kipo kituo cha utafiti wa Mifugo Naliendele, Mtwara.

Kwa upande wao wafugaji wa kuku kutoka kijiji cha Nandagala walionufaika na Mradi huo, waliopata kuku 25 wapo nane, waliopata kuku 50 wapo nane na waliopata kuku 75 wapo nane na kufanya jumla ya watu 24 waliopatiwa kuku aina ya Saso na Tanbrow Juni 6, 2024.

> **Mimi niwaambie tu yakwamba hili jambo si dogo na lina manufaa makubwa sana kwenu, soko la kuku wa nyama na mayai halijawahi kujaa**
>
> **Mhe. Chikongwe**

Kuku aina ya Saso na Tanbrow wana uwezo wa kutaga mayai 270 - 300 kwa kila kuku mmoja kwa mwaka na ukomo wa kutaga mayai ni miaka miwili.

Kwa upande wake, Daktari wa Mifugo Kata ya Nandagala Jenifer Moses amesema ili kudumisha ufugaji wa kuku kuna haja ya kuwa na Kituo cha utafiti wilayani Ruangwa kwasababu itasaidia kupunguza gharama kwa mfugaji endapo mfugo utapata homa na kuhitajika kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Naye, Mtendaji wa Kata ya Nandagala Bi Awesa Rashidi ametoa wito kwa wananchi kufuga kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji wa kuku na kuendeleza ufugaji huo kwani ni mtaji katika familia.

# Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam Tawi la Ruangwa Kukamilika Ndani ya Miezi 18

*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambaye ni Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya kiuchumi Profesa Bernadeta Killiani akiwa kwenye kikao cha uzinduzi wa kamati ya KASEMA, leo Julai 9, 2024 . amesema kwamba Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam tawi la Ruangwa watahakikisha ndani ya miezi 18 Mkandarasi anakabidhi majengo. picha na mpiga picha wetu.*





Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambaye ni Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumi Profesa Bernadeta Killiani amesema kwamba Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam tawi la Ruangwa watahakikisha ndani ya miezi 18 Mkandarasi anakabidhi majengo.

Ameyasema hayo leo Julai 9, 2024 katika Kikao kazi cha uzinduzi wa Kamati ya "Kasema" itakayoshirikiana na Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumi kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri.

Aidha, Profesa Killiani ametoa wito kwa wananchi wa Ruangwa kuonesha ushirikiano kwani mafanikio ya Mradi yanategemea muamko na ushirikiano na wanachi wa eneo husika.

Kamati ya "Kasema" ina Wajumbe watano na ina lengo la kukusanya na kushughulikia maoni au malalamiko ya wananchi katika eneo husika kuhusu Mradi. Pia, ina lengo la kuweka kumbukumbu za kile kinachofanyika katika Mradi, na ni sehemu ya Ulinzi na Usalama wa Mradi huo.

Mradi wa Elimu ya Juu kwa mageuzi ya Uchumi chini ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam umefadhiliwa na Mkopo wa Benki ya Dunia na utekelezaji wake ni katika maeneo mapya 14, na mpaka sasa maeneo mapya matatu tayari yameshafikiwa ambayo ni Ngongo (Lindi Manispaa), Likunja (Wilaya ya Ruangwa) pamoja na Kagera.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ameushukuru Uongozi wa Kata ya Likunja kwa kutoa Hekari 400 ambapo Kitivo cha Kilimo kitajengwa.

Aidha, Mhe Chikongwe ameendelea kwa kusema kuwa Mradi huu ni chachu ya maendeleo wilayani Ruangwa kwa sababu wananchi watajifunza namna ya kuongeza uzalishaji, idadi ya watu pia itaongezeka na hii itaenda kubadili sura ya Wilaya ya Ruangwa.

Pia, ametoa wito kwa wakazi wa Kata ya Likunja wajenge nyumba bora na za kisasa, kulima vizuri na kisasa zaidi ili kuongeza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Halmashauri kwa ujumla







# Mkuu wa Mkoa wa Lindi Awaombea Dua Wafanyabiashara Ruangwa



*Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainab Telack*

Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainab Telack amewaombea Dua Wafanyabiashara wa Wilaya ya Ruangwa leo Julai 12, 2024 katika Kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Chama Cha Walimu Ruangwa, ikiwa ni ziara yake ya kwanza baada ya kutoka ibada ya kuhiji katika mji mtukufu wa Makka

Aidha, Mhe. Telack ametoa wito kwa Wafanyabiashara hao kufanya kazi zao kwa uadilifu na uaminifu na kuhakikisha mazingira yao ya biashara yanakuwa mazuri ili kuvuta wateja zaidi.

“Hakuna kazi rahisi, kazi rahisi ni ile ya mwenzako tu, kwahiyo boresheni mazingira yenu ya kazi kwa kuyafanya usafi na nyinyi wenyewe kuwa na kauli mzuri za kuwavuta wateja zaidi” Amesema Mhe. Telack.

**TANGAZA NASI RUANGWA FM 88.4**

**Email: ruangwafmradio@gmail.com**
**Phone: +255718137626**

88.4 RUANGWA FM Sauti ya kweli

## Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Akagua Kituo cha Askari wa Uhifadhi Wanyamapori Ruangwa

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dunstan Kitandula, ametembelea na kukagua kituo cha Askari wa uhifadhi wanyamapori leo Julai 17, 2024, kilichojengwa katika kijiji cha Machang’anja, Wilaya ya Ruangwa.

Kituo hicho kimejengwa kwa ajili ya kutoa msaada wa haraka kwa wananchi, ikiwemo kuimarisha ulinzi na kutoa elimu dhidi ya wanyama pori wanaovamia makazi ya watu, hususani tembo. Kituo kitahudumia Kata tatu zinazo kizunguka ambazo ni Makanjiro, Narungombe, na Mandawa.

Aidha, Mhe. Kitandula amezungumza na wananchi wa Kijiji cha Machang’anja, na amewahakikishia kuwa Serikali imejipanga vizuri kuleta suluhisho la kudumu kuhusu tatizo la tembo. Amewahimiza wananchi kutumia kituo hicho ipasavyo kwa kuwa kimejengwa kwa ajili ya kuwasaidia.

“Serikali imejipanga kununua helikopta mbili zitakazotumika katika zoezi la kuondoa tembo karibu na makazi ya watu. Kwa Wilaya ya Ruangwa, Serikali italeta mabomu 400 ya kufukuza tembo na kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu namna ya kujilinda dhidi ya tembo. Pia, italeta mipira yenye kelele za kukera na vifaa maalum vya kutupa mabomu ili askari wasitumie mikono,” alisema Mhe. Kitandula.



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dunstan Kitandula (Kulia), ametembelea na kukagua kituo cha Askari wa uhifadhi wanyamapori leo Julai 17, 2024, kilichojengwa katika kijiji cha Machang’anja, Wilaya ya Ruangwa. Picha na mpiga picha wetu*

“ Ninapata machungu kama mnayopata ninyi maana naelewa nini mnapitia kwa wakati huu

## *DONDOO ZA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI*


# Kumbuka Kujiandikisha Kuwa Mpiga Kura, Ndio Msingi wa Utawala Bora















# Matukio Katika Picha



*Afisa Afya wa Wilaya ya Ruangwa, Bi. Blandina Lukindo, akigawa dawa za kutibu na kusafisha maji ya kunywa (Waterguard) kwa Wenyeviti wa vitongoji vya Kijiji cha Nanjaru, kata ya Nambiranje, kwa ajili ya kugawa kwenye kaya zote. Zoezi hilo limefanyika leo, Julai 7, 2024, kama sehemu ya juhudi za kujikinga na magonjwa ya mlipuko. Picha na mpiga picha wetu.*



*Bi. Tolage kutoka Wizara ya Afya wa pili (kushoto) akiwa ameambatana na Uwakilishi wa Ofisi ya Mganga Mkuu Mkoa wa Lindi wakiwa katika zoezi la kuwachagua wahudumu wa afya ngszi ya jamii. Kila Mwananchi wa Ruangwa asiyepungua umri wa miaka 18 au usiozidi miaka 55 ana sifa ya kuomba nafasi na mwisho wa maombi ni siku ya Jumatatu tarehe 21,Julai, 2024.*




*Washauri wa Kampuni ya Carbon First wakiongozwa na Bi. Lilian Rushango wamefanya mazungumzo na Viongozi wa vijiji vya Chingubwa, Mchichili, Nahanga na Mtondo wilayani Ruangwa. Mazungumzo hayo yamefanyika leo Julai 16, 2024 katika Ofisi za vijiji hivyo na yalihusisha maswali kutoka kwa washauri wa kampuni hiyo na maoni ya Viongozi wa vijiji kuhusu jinsi ya kuilinda na kuitunza misitu ya vijiji hivyo kabla ya kuanza biashara ya hewa ukaa katika Wilaya ya Ruangwa.*



*Moja ya shamba la Mkulima wa mboga mboga lililopo kata ya Nandagala Mkulima huyo anayetegemea kilimo kujikwamua kiuchumi. Kijiji cha Namahema B kilichopo Kata ya Nandagala wilayani Ruangwa shughuli kuu inayofanywa na wakazi wa hapa ni kilimo. Kijiji cha Namahema B kina jumla ya wakulima 215 ambapo wakulima wa mbogamboga ni 86, wakulima wa Korosho ni 40 na wakulima wa mazao ya chakula ni 89.*

# Kongamano la Kukusanya Maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 Wilaya ya Ruangwa Lafanyika Leo



*Wadau wa maendeleo na makundi mbalimbali ya wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wakitoa maoni yao kwenye kongamano la ukusanyaji wa maoni ya Dira ya Taifa ya maendeleo ya mwaka 2050. Aidha wameeleza matamanio yao kuhusu namna wanavyotamani kuiona Tanzania ifikapo mwaka 2050. Kongamano hilo limeonyesha jinsi ambavyo Serikali inathamini maoni ya wananchi katika mipango ya maendeleo ya Taifa. Ushirikishwaji huo ni muhimu kwa kuhakikisha kwamba mipango inayowekwa inakidhi mahitaji halisi ya jamii na kuchangia katika kujenga Tanzania yenye ustawi na maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2050.*

Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imefanya kongamano maalum la ukusanyaji wa maoni kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Kongamano hilo, limewakutanisha watu kutoka makundi mbalimbali katika jamii na limefanyika leo, Julai 29, 2024, katika ukumbi wa mikutano wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 inalenga kuendeleza mafanikio ya Dira ya 2025 na kuleta maendeleo endelevu kwa muda mrefu. Malengo ya Dira ya 2050 ni pamoja na kukuza uchumi wenye ushindani kimataifa, kuongeza ustawi wa jamii, kuimarisha miundombinu, huduma za kijamii, na kulinda mazingira. Serikali inashirikisha wadau mbalimbali katika mchakato wa kuandaa mpango huo ili kuhakikisha kuwa unakidhi mahitaji na matarajio ya Watanzania.

Aidha, Wadau wa maendeleo na makundi mbalimbali ya wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wamejitokeza na kutoa maoni na matamanio yao kuhusu namna wanavyotamani kuiona Tanzania ifikapo mwaka 2050. Baadhi ya maoni hayo ni pamoja na; kuwekeza katika Teknolojia kuanzia shule za msingi hususani katika matumizi ya tehama, kutoa huduma za afya bure kwa wajawazito ifikapo 2050, kuongeza wataalamu katika sekta ya kilimo kuanzia ngazi ya kijiji, kudumisha zaidi amani na usalama wa Taifa ili nchi izidi kuwa salama, kupunguza bei ya gesi na umeme ili Watanzania wote watumie nishati safi ifikapo 2050, Kuwe na gredi ya Taifa ya maji kama ulivyo umeme, kuongeza ajira kwa vijana ili kuwaokoa na janga la madawa ya kulevya, na Taifa lijikite kwenye uwekezaji wa viwanda ili kuongeza soko la ajira.

Ikumbukwe, Kongamano hilo limeonyesha jinsi ambavyo Serikali inathamini maoni ya wananchi katika mipango ya maendeleo ya Taifa. Ushirikishwaji huo ni muhimu kwa kuhakikisha kwamba mipango inayowekwa inakidhi mahitaji halisi ya jamii na kuchangia katika kujenga Tanzania yenye ustawi na maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2050.



# Vijiji Vyote 90 vya Wilaya ya Ruangwa Vina Umeme Sasa

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe, ametangaza kwa furaha kwamba vijiji vyote 90 vya Wilaya ya Ruangwa sasa vina umeme, ameyasema hayo Leo, Julai 29, 2024 akiwa katika ukumbi wa mikutano wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya, alipokuwa akichangia maoni kwenye kongamano la ukusanyaji wa maoni ya Dira ya Taifa ya maendeleo ya mwaka 2050.

Aidha,Mhe. Chikongwe ameeleza kuwa hatua hii ni muhimu kwa maendeleo ya jamii na ametoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa kutekeleza mradi huu mkubwa ambao utaongeza fursa za kiuchumi, elimu, na afya kwa wananchi. Umeme huo utachangia kuboresha hali ya maisha na kuleta maendeleo endelevu katika Wilaya ya Ruangwa.

Hatua hii inawakilisha mwanzo wa mapinduzi makubwa katika maisha ya wananchi wa Ruangwa, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika eneo hilo.

## Wazazi Wilaya ya Ruangwa Wasisitizwa Kuwapa Watoto Wao Elimu





Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ametoa wito kwa wazazi kuwasomesha watoto kwa manufaa yao na familia zao.

“Wazazi tujitahidi kusomesha watoto wetu kwani ni faida kwetu na ni msaada mkubwa sana kwetu na ulimwengu wa sasa elimu ni muhimu kwasababu teknolojia inakua kila siku hivyo kama mtoto hajapata elimu atapata tabu sana kwa kizazi tulichopo” Amesema Chikongwe.

Ameyasema hayo leo Julai 28, katika Kikao cha kuhamasisha elimu Kata ya Nandagala kilichofanyika katika shule ya Msingi Mkata iliyopo kijiji cha Namahema “A” Kata ya Nandagala, wilayani Ruangwa.

Aidha, Mhe. Chikongwe amewashukuru wanakikundi cha wasomi wazawa wa Wilaya ya Ruangwa (Ruangwa Graduates Platform) kwa moyo wao wa kujitoa kwa ajili ya wilaya yao na Taifa kwa ujumla.

Kikundi cha wasomi wazawa wa Wilaya ya Ruangwa (Ruangwa Graduates Platform) kimeanzishwa mnamo mwaka 2021 kikiwa na wanakikundi zaidi ya 12 kinachoongozwa na Mwenyekiti Bi. Madina Mkundi kikiwa na lengo la kuhamasisha masuala ya Elimu, Afya na masuala mbalimbali ya kijamii.

Kwa upande wao wanakikundi cha wasomi wazawa wa Wilaya ya Ruangwa wametoa mafunzo mbalimbali na ushuhuda kwa yale yote waliopitia na kuwasihi wazazi na Wanafunzi walioudhuria mkutano huo kutilia mkazo suala la Elimu kwani kwa ulimwengu wa sasa Elimu ni zaidi ya mkombozi.

OFISI YA MKURUGENZI
**Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa**

## TANZIA



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu **Frank Fabian Chonya**, anasikitika kutangaza kifo cha Mwalimu **Grace Ntila** wa Shule ya Msingi Namakonde kilichotokea leo tarehe 30 Julai 2024, asubuhi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alipokuwa anapatiwa matibabu.

Taarifa zaidi kuhusu **mazishi**, tutaendelea kujulishwa.



Bwana ametoa, Bwana ametwaa
Jina lake lihimidiwe.

ruangwadc    www.ruangwadc.go.tz

**kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi. [Mwanzo 3:19]**

Wilaya ya Ruangwa imeanzishwa mnamo mwaka 1995 wakati wa Raisi wa awamu ya pili Hayati Ally Hassani Mwinyi, nakuzinduliwa rasmi mwaka 1999 wakati wa Raisi wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa.

Wilaya ya Ruangwa inapatikana ndani ya Mkoa wa Lindi katika majira nukta -10.0809° S, 38.9401° E ipo umbali wa kilometa 150 kutoka makao makuu ya Mkoa , ina Vijiji 90, Kata 22, Vitongoji 150 na idadi ya watu wapatao 185,573, kati ya hao 91,469 ni Wanaume na 94,104 ni Wanawake kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 .

# TIMU YA WAHARIRI

## WAHARIRI

MPETA KOBA
NYAMBITA MAGOMA

## MPIGA PICHA

MPETA KOBA

## MWANDISHI

ADELINA KASPALI

## MSANIFU KURASA

NYAMBITA MAGOMA




# JARIDA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

**Ruangwa kwa Mendeleo Inawezekana Timiza Wajibu wako**

ruangwadc

www.ruangwadc.go.tz

ruangwadc

Limeandaliwa na kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa
Barua pepe: ded@ruangwadc.go.tz
Tovuti: www.ruangwadc.go.tz
S.L.P 51, Ruangwa
Fax: +25532933212

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA